

PAMBANO KUU

Kwa Nini Mungu Alimuumba Lusifa?

Ingawaje Biblia inavidokezo vichache kuhusu Swali hili, bado hata hivyo haiwezekani kulitolea jibu linalotosheleza katika ukamilifu wake. Mada hii haijashughulikiwa kwa uwazi...

ÁNGEL MANUEL RODRÍGUEZ

2026

Ikiwa Mungu alijua kwamba Lusifa angeasi, kwa nini alimuumba?

Ingawaje Biblia inavidokezo vichache kuhusu Swali hili, bado hata hivyo haiwezekani kulitolea jibu linalotosheleza katika ukamilifu wake. Mada hii haijashughulikiwa kwa uwazi na kwa kina cha kutosha katika Biblia. Kwa kawaida maswali kama haya yanabeba ndani yake hofu kwamba Mungu anaweza kuhusishwa kwa namna fulani na asili ya dhambi na uovu katika ulimwengu. Hapa yako mambo machache ya kutafakari kuhusiana na vidokezo vichache vya kimaandiko na vinavyotoa majibu kwa kiasi flani kuhusu swali hili:

1. Kuna Uhusiano gani kati ya Mungu na Uovu?

Linapokuja suala la asili ya dhambi na uovu Biblia haikubaliani na fundisho linaloitwa monism—Monism inafundisha kwamba Mungu ndiye mwanzilishi wa mema na mabaya; yote mawili.— Lakini hata hivyo tunajua kwamba wema na ubaya ni kanuni mbili ambazo tangu wakati uovu ulipojitokeza zimekuwa zikipigana daima. Mahali pazuri pa kuanzia ni kujua kuwa Biblia inakanusha kabisa kwamba dhambi na uovu vilikupo milele, na inakanusha kwa kuthibitisha kwamba matukio kama hayo yalikuwa na mwanzo na pia yatakuwa na mwisho. Kwa kuwa Mungu ni wa milele na dhambi na uovu si vya milele, tunaweza kuhitimisha kwamba dhambi na uovu havina asili wala chanzo chake katika Mungu. Mtu mwingine anaweza kuheoji: Je, upo uwezekano kwamba dhambi na uovu havikuwepo milele lakini Mungu alipoumba aliumba wema na ubaya kwa pamoja na hivyo vinakuwa sehemu ya shughuli ya uumbaji wa Mungu? Jibu la kibiblia liko wazi: Kila kitu ambacho Mungu aliumba

"kilikuwa chema sana" (Mwa. 1:31). Pia Biblia inafundisha kwamba Mungu 'Yeye Mwamba, kazi yake ni kamilifu; Maana, njia zake zote ni haki. Mungu wa uaminifu, asiye na uovu, Yeye ndiye mwenye haki na adili. '(Kum 32:4). Hii inathibitisha kwamba wakati Mungu alipoumba, hakuumba uovu, na hawezi kuhusishwa kwa namna yoyote ile na kuwepo kwake.

2. Uhusiano wa Mungu na Lusifa: Vipi kuhusu Lusifa?

Ukweli ni kwamba Mungu alimuumba Lusifa. Biblia inasema mambo matatu muhimu kumhusu. Kwanza, yeye ni kiumbe; pili, wakati Mungu alipomuumba hakuwa na upungufu, bali alikuwa "mkamilifu"; na tatu, "uovu ulipatikana ndani yake" (Ezek. 28:15). Maandiko yanathibitisha wema na ukamilifu wa uumbaji wa Mungu (katika kumuumba Lusifa) huku pia yakitambua kwamba kitu kibaya kilitokea kwa kiumbe huyu ("uovu ulipoonekana ndani yako"). Lakini, je, sehemu ya mwisho ya andiko haionyeshi kitu kibaya ambacho huenda kilikuwa ndani ya Lusifa tokea mwanzo na ambacho wakati fulani baadaye kilikuja kuonekana wazi?

Hapa tunakabiliwa na siri au fumbo ambalo jibu lake linapaswa hasa kufafanua asili hasa ya dhambi. Wakati hali ya ukamilifu wa kerubi huyu kunaelezwa wazi kama matokeo ya uumbaji wa Mungu, uovu haukua moja ya mipango ya Mungu. Uovu ulikuja kama mvamivi asiye na sababu wala kisingizio. Hatuelezwi katika maandiko namna Lusifa alivyohama kutoka katika utakatifu wa tabia mpaka kuruhusu uovu kuingia moyoni mwake, na hili bila shaka Mungu ameliacha hivyo ili tujifunze kumwamini kwa kuzingatia kile tunachokiona katika tabia yake ya upendo na namna ambavyo anahusiana na sisi siku kwa siku. Maelezo makini yenye uvuvio katika kitabu kinachoitwa Pambano Kuu

(The Great Controversy) yanasema: “Hakuna upungufu wowote uliojitokeza katika utawala wa Mungu uliopelekea kuibuka kwa dhambi. Dhambi ni mvamizi, ambaye uwepo wake hauwezi kupata sababu ya msingi. Ni fumbo, ni kama kitendawili kisicho na jibu; kuitafutia sababu ni kuitetea. Ikiwa sababu ya kuwepo kwake ingepatikana au kuonyweshwa, ingelikoma kuitwa dhambi tena. Maelezo tuliyonayo juu yake ni yale yanayopatikana katika maandiko matakatifu; ni “uasi wa sheria;” ni vita ya tamaa ya uvunjifu wa sheria dhidi ya kanuni ya upendo ambayo ni msingi wa utawala wa ufalme wa Mungu.” *{The Great Controversy 492.2}*

Jambo jingine tunaloelezwa ni namna uzuri na hekima yake vilivyokuwa moja ya sababu za kuanguka kwake (Ezekieli 28:17). Lakini bado maandiko hayaelezi namna alivyohama kutoka kuutumia uzuri na hekima yake kumtukuza Mungu na kuanza kuvitumia kumuasi Mungu. Hilo ni fumbo ambalo kwa sasa hatujapewa majibu yake.

Tuliyofunuliwa kwa sasa ni kwamba Mungu hakuhusika kuanzisha uovu au kusababisha uovu uwepo. Na tunachohitajika kufanya kwa sasa ni kuchagua kwa hiyari kumwamini na kumpenda kama mwitikio wa uchaguzi wa viumbe vyenye utashi, kutokana na vile tunavyoona upendo wa Mungu ukidhihirika kwetu. Kuna mengi ambayo kwa sasa hajatolewa ufafanuzi wa wazi, lakini yale tuliyonayo, ambayo yamewekwa wazi, yanatutosha kabisa kwa ajili ya wokovu wetu na yanatosha kabisa kujenga imani yetu kwa Mungu.

3. Kuchunguza-chunguza Akili ya Mungu:

Ukweli kwamba Mungu anajua yote inaweza ikamaanisha kwamba alijua mapema kwamba Lusifa, angekuwa Shetani na mshtaki hapo mbeleni.

Na mtu anaweza kusema kwa kuwa Mungu ni muweza wa yote, dhambi na uovu vipo kwa sababu Mungu anaviruhusu kuwepo. Kwa nini aliruhusu vyote kuwepo? Bila shaka Hilo nalo ni swali lako pia. Wapo wanateolojia ambao wamejaribu kuweka tofauti kati ya asili ya Lusifa na utashi wake–wanachojaribu kusema ni kwamba, Lusifa alikuwa mkamilifu na chanzo cha yeye kutumia utashi wake vibaya kilitokana na jambo jingine nje yake yeye mwenyewe–. Jambo hilo linauelekeo pia wa kumlaumu Mungu kwamba alipaswa kumuumba Lusifa bila uwezekano wa kuichagua dhambi. Katika hili tunahitaji kufahamu kuwa Lusifa akiwa katika asili yake ya awali, kama ilivyoumbwa na Mungu, alikuwa mkamilifu (mwenye utimamu wa kila namna); lakini utashi wake (utimamu wake kiakili), kama uhuru uliotumika vibaya, na kusababisha dhambi na uovu havikuwa matokeo ya uumbaji mbaya wa Mungu. Mungu aliwajibika kwa kazi ya kwanza ya kuumba kilicho kikamilifu na si kwa tukio la pili la matumizi mabaya ya uhuru wa kuchagua. Matumizi mabaya ya utashi wa Lusifa yalitegemea, lakini hayakuamuliwa na, uhuru ambao Mungu aliwekeza ndani ya viumbe vyake vyenye akili.

Lakini Je, Mungu asingeweza kuepuka yote hayo kwa kutokumuumba Lusifa? Gharama kwake ingekuwa kubwa sana, kwa kiasi ambacho kwa kweli hakiwezi kufikirika. Wakati fulani katika umilele Mungu aliamua kuumba viumbe wenye akili, huru. Mungu katika ufahamu wake wote alijua kwamba moja kati ya viumbe hao angeasi dhidi yake. Je, sasa hapaswi wakati huo kubadili mpango wake? Jibu la asili la mwanadamu litakuwa, "Ndiyo!" Tungeacha mpango wetu kwa sababu tungeogopa kukabiliwa na shida mbaya kama hiyo. Kwa kufanya hivyo shida iliyotarajiwa ilitushinda kwa kutulazimisha kubadili mpango wetu.

Lakini Mungu si kama sisi! Mara tu alipoamua kuumba, hakuna nguvu halisi au uwezekano wowote ambao ungemlazimisha kubadilisha

mpango Wake. Vinginevyo, hofu ya dhambi ingemshinda hata kabla ya kuumba chochote. Mungu ni asiye na woga, ambaye, bila kubadilisha mpango Wake, aliamua kukabiliana na tatizo la dhambi na uovu na kulitatua kupitia kwa Yesu Kristo. Huenda aliwaza hivyo! Nani anajuaye?

Muhimu tu ni kwamba, ameahidi ataukomesha uovu na hautajitokeza tena milele na milele huo mbeleni (Nahumu 1:9)

Ni muhimu kuzilinda nafsi zetu na hali flani za mashaka juu ya Mungu zinazobeba ndani yake hali ya kutafiti na kuchunguza zaidi ya mipaka ya yale yaliyofunuliwa kwetu. Tunayoyafahamu kwa sasa, yanatosha kabisa kwa ajili ya wokovu wetu.

KUMB. 29:29

> 'Mambo ya siri ni ya BWANA, Mungu wetu; lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele, ili tuyafanye maneno yote ya sheria hii.'

Source: Sehemu kubwa ya makala hii imechukuliwa kutoka **Biblical Research Institute**.



Pakua Kitabu hiki kidogo kinachofafanua zaidi juu ya Fundisho la Biblia kuhusu kwa nini Mungu hakumuua Shetani mara uovu ulipotokea? na Kwa nini kuna uovu duniani wakati Mungu ni mwema kabisa? Kitabu hiki kimeandikwa na Mchungaji Almodad Amos Yaragwiller. Pakua sasa PDF ...

Soma na upakue “Pambano Kuu” (PDF) →

Zaidi kutoka Injili Milele

Makala, vitabu, video na sauti zaidi zinapatikana kwenye maktaba ya Injili Milele:

Je, Sabato Ilikoma kwa Kuwa Ilikuwa Kivuli cha Mambo Yajayo?
Sabato · PDF

Sanduku la Agano: Je, Litaonekana Tena?
Unabii · PDF

Nini Hasa Maana ya Kibiblia ya Maneno ya Baba: “Mimi Leo Nimekuzaa”?
Uungu · Video

Je, Yesu ni “Mungu Mwana” au “Mwana wa Mungu”?
Uungu · Video

Papa Gregory XIII Alipobadilisha Kalenda: Siku Zilivurugwa, Sabato Ilipotea?
Sabato · PDF

Je, ni Lazima Kupiga Magoti Wakati wa Maombi?
Ibada · PDF

Injili Milele

almodad-2.github.io/injili-milele/sw/

WhatsApp +255 718 834 621 · modaofhope@gmail.com

© 2026 Pr. Almodad Amos Yaragwiller · Injili Milele. Haki zote zimehifadhiwa. Usiuze nakala hii bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi.